

# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM

**PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO**

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com



## MATANGAZO – SIKUKUU YA FAMILIA TAKATIFU - 28.12.2025

| | | |
|---|---|---|
| 1. | LEO DOMINIKA<br>28.12.2025 | **SIKUKUU YA FAMILIA TAKATIFU**<br>Mchango wa pili ni kwa ajili ya ujenzi |
| 2. | JUMATANO<br>31.12.2025 | Tunaalikwa wote kushiriki usafi Kanisani na mazingira yake saa 1:00 asubuhi mara baada ya Misa. |
| 3. | JUMATATO<br>31.12.2025 | **MISA YA SHUKRANI KWA MUNGU**<br>Kwa kuhitimisha mwaka 2025 salama, itaanza saa 4:00 usiku.<br>Jumuiya ya Mt. Silvesta itatoa shukrani kwa heshima ya Msimamizi wao (31 Desemba). |
| 4. | ALHAMISI<br>01.01.2026<br>MWAKA MPYA 2026 | **SHEREHE YA BIKIRA MARIA MTAKATIFU MAMA WA MUNGU**<br>Misa ya kuomba Baraka za Mungu kwa Mwaka Mpya saa 2:00 asubuhi |
| 5. | IJUMAA<br>02.01.2026 | Kumbukumbu ya Mt. Basili Mkuu, Msimamizi wa Kanda A |
| 6. | JUMAMOSI<br>03.01.2026 | Kumbukumbu ya Jina Takatifu la Yesu.<br>Jumamosi ya Kwanza ya Mwezi, Misa saa 3:00 asubuhi kwa heshima ya Moyo Safi wa Maria.<br>Kanda A Mt. Basili Mkuu watatolea vipaji na kusimamia kwa heshima ya Msimamizi wao.<br><br>Misa katika Jumuiya ya Mt. Stefano Shahidi kwa heshima ya Msimamizi wao saa 10:00 jioni. |
| 7. | DOMINIKA<br>04.01.2026<br><br>DOMINIKA YA KWANZA YA MWEZI, HITIMISHO MCHANGO WA MAENDELEO WA DESEMBA 2025 NA<br><br>DOMINIKA YA ZAKA | **SHEREHE YA TOKEO LA BWANA, EPIFANIA**<br><br>**Misa ya 1: Saa 12:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Yosefu Mfanyakazi<br>Watangaza Neno: Emmanueal Raphael na Ester William<br><br>**Misa ya 2: Saa 2:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Kizito<br>Watangaza Neno: Levina Mshana na Angela Komba<br><br>**Misa ya 3: Watoto**<br>Wasimamizi: Mt. Yosefu Mfanyakazi na Mt. Kizito<br><br>Mchango wa pili ni kwa ajili ya ujenzi |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | MISA YA DARAJA YA USHEMASI | Jumamosi 03.01.2026 itafanyika Misa ya kutoa Daraja ya Ushemasi kwa Mashemasi 12 katika Viwanja vya Msimbazi Center itakayoanza saa 3:00 asubuhi. Askofu Mkuu anatukaribisha waamini wote kushiriki. |
| 9. | KUHITIMISHA MWAKA WA JUBILEI KUU KIJIMBO | Misa ya kuhitimisha Jubilei Kuu 2025 na kuwakumbuka wafia dini wa Pugu itaadhimishwa katika Kituo cha Hija Pugu Jumamosi 10.01.2026 kuanzia saa 3:00 asubuhi. Tunaalikwa sote kushiriki. |
| 10. | UTOTO MTAKATIFU | Tunawapongeza Watoto wa Utoto Mtakatifu 37 na walezi 3 walioshiriki Misa ya Kumbukumbu ya Watoto Mashahidi jana.<br><br>Kutakuwa na Kongamano la shukrani la Utoto Mtakatifu Dekania litakalofanyika Parokia ya Mpiji Magohe, Jumamosi ijayo tarehe 03.01.2026. Gharama ya kushiriki ni Sh. 3,000/= bila usafiri. Watoto watakaoshiriki mwisho wa kulipia ni Alhamisi 01.01.2026.<br><br>Jumuiya zinakumbushwa kuchagua walezi wawili, mwanamme na mwanamke kuwa walezi wa Utoto Mtakatifu. |
| 11. | MISA YA UFUKWENI VIJANA | Pongezi kwa Vijana 83 walioshiriki Misa ya Ufukweni (Beach Mass) kiparokia kule Bagamoyo jana. Tunaomba mwamko huo uendelee katika matukio yote ikiwepo Semina na mafungo kwa mwaka 2026. |
| 12. | RATIBA YA USAFI, USIMAMIZI NA VIPAJI 2026 | Ratiba ya Usafi, kusimamia Misa na vipaji kwa mwaka 2026 imetoka tunaombwa kuizingatia. Kalenda ya matukio yote Parokia itakamilishwa baada ya kupata Kalenda ya Jimbo. |
| 13. | MISA KWA HESHIMA YA WASIMAMIZI WA JUMUIYA NA KANDA | Jumuiya na Kanda zinazopenda kuadhimisha Misa kwa heshima ya wasimamizi wao zinatakiwa kuwasilisha tarehe tarajiwa ya Misa ofisini au kwa makatibu kabla ya 10.01.2026. |
| 14. | MAJITOLEO KWA WAHITAJI NOELI | Tunawashukuru wote waliojitolea vitu mbalimbali na vyakula kwa ajili ya wahitaji kwa sherehe ya Noeli. Mungu awazidishie. |
| 15. | GAZETI LA TUMAINI LETU | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5. |

***Kauli Mbiu ya Mwaka wa Jubilei Kuu: "Jubilei 2025 – Mahujaji wa Matumaini."***

## MWAKA MPYA

| | | |
|---|---|---|
| MISA YA MKESHA | MISA YA SHUKRANI<br>ITAANZA SAA 4:00 USIKU<br>31.12.2025 | **WASIMAMIZI** – UWAKA<br>- WATANGAZA NENO<br>1. MARY NYAKI<br>2. CASTO SIMPLIS |
| MISA YA MWAKA MPYA<br>01.01.2026<br>ASUBUHI | - SHEREHE YA MARIA MTAKATIFU MAMA WA MUNGU<br>- SIKU YA KUOMBEA AMANI<br>MISA ITAANZA SAA 2:00 ASUBUHI | **WASIMAMIZI** – WAWATA<br>- WATANGAZA NENO<br>1. PANCRASIA SHIRIMA<br>2. BAPTIS KOMBA |

## TANGAZO LA DARAJA YA UPADRE KWA MARA YA PILI

1. Mhashamu Sana Askofu Mkuu Jude Thaddaeus Ruwa'ichi OFMCap. Wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam anatangaza Daraja ya Upadre wa **Shemasi Edson Mwoleka CSC wa Shirika la Wamisionari wa Msalaba Mtakatifu** (Congregation of the Holy Cross) anatoka katika Parokia ya Roho Mtakatifu, Kitunda, Jimbo Kuu la Dar es Salaam. Anatarajiwa kupewa Daraja Takatifu ya Upadre tarehe 18.01.2026 katika Kanisa la Moyo Mtakatifu wa Yesu, Parokia ya Sombetini, Jimbo Kuu la Arusha.

2. Mhashamu Sana Askofu Mkuu Jude Thaddaeus Ruwa'ichi OFMCap. Wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam anatangaza Daraja ya Upadre wa **Shemasi Yohannes Gerald Mfilinge C.PP.S wa Shirika la Wamisionari wa Damu Azizi** (The Society of Preciuos Blood) anayefanya mazoezi ya kichungaji katika Parokia ya Mt. Nicholaus, Kunduchi katika Jimbo Kuu la Dar es Salaam. Anatarajiwa kupewa Daraja Takatifu ya Upadre tarehe 24.01.2026 katika Kanisa la Mwenyeheri Bakanja, Parokia ya Boko, Jimbo la Bagamoyo.

Tuwaombee waifikie Daraja hiyo wanayoitamani.

### MISA YA MKESHA WA MWAKA MPYA TAR. 31.12.2025 SAA 4:00 USIKU

| | |
|---|---|
| SOMO I | Isa 12:1-6 |
| WIMBO WA KATIKATI | Zab 92:1-8 (K)1 |
| SOMO II | 1Thes 5:12-25 |
| SHANGILIO | Ebr 1:1-2 |
| INJILI | Lk 17:11-19 |

### MASOMO YA DOMINIKA – TOKEO LA BWANA, EPIFANIA - 04.01.2026

| | |
|---|---|
| SOMO I | Isa 60:1-6 |
| WIMBO WA KATIKATI | Zab 72:1-2, 7-8, 10-13 (K)11 |
| SOMO II | Efe 3:2-3, 5-6 |
| SHANGILIO | |
| INJILI | Mt 2:1-12 |